

MAENEO MAKUU YA HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII

Huduma za Ustawi wa Jamii nchini zinatolewa kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo Mbalimbali. Kwa kuzingatia sheria zilizopo na muundo wa huduma za Ustawi wa jamii zinazotolewa nchini zimegawanyika katika Maeneo Makuu matatu ambayo ni;

i. Ustawi wa familia, watoto, malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto

Huduma zitolewazo katika eneo hili ni:

- i. Huduma za usuluhishi wa ndoa zenye mifarakano na matunzo ya watoto
- ii. Huduma ya matunzo kwa watoto wanaozaliwa nje ya ndoa
- iii. Huduma ya makao ya watoto na walio katika mazingira hatarishi
- iv. Huduma ya malezi ya kambo na kuasili
- v. Huduma ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto wadogo
- vi. Huduma ya malezi , matunzo na ulinzi shirikishi jamii kwa watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi
- vii. Huduma kwa familia zenye dhiki
- viii. Kuratibu na kuunda kamati za ulinzi wa wanawake na watoto katika ngazi zote, (Mitaa, Kata na Halmashauri).

ii. Marekebisho ya tabia na haki za mtoto kisheria.

Huduma zitolewazo katika eneo hili ni pamoja na:

- i. Kuwezesha watoto kwenda shule ya maadilisho kwa amri ya Mahakama
- ii. Kuwaunganisha Waadiliwa na huduma muhimu kama vile elimu ya msingi, stadi za aisha na ushauri nasihi,
- iii. Kufanya utengamao kwa Waadiliwa na kuwaunganisha na familia/jamii zao
- iv. Kuwatambua watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani na kuwaunganisha na familia zao au kuwaunganisha na mpango wa marekebisho ya tabia
- v. Kufanya unasihi na kutoa msaada wa kisaikolojia kwa Waadiliwa ili kusaidia kurekebisha tabia zao
- vi. Kutoa rufaa kwenda kwenye mpango wa marekebisho ya tabia
- vii. Kuhakikisha watoto wanaoshitakiwa kwa makosa ya jinai wanapelekwa katika mahakama za watoto

- viii. Kuhakikisha watoto wanapelekwa katika mahabusi za watoto badala ya Mahabusi za watu wazima pale ambapo wamekosa dhamana au makosa yao hayastahili dhamana
- ix. Iwapo watoto wamepatikana na hatia kwa kosa la jinai na iwapo umri wao ni chini ya miaka 16, Afisa Ustawi wa jamii atawasilisha taarifa mahakamani ili kumuwezesha Hakimku kupata picha kamili kuhusu Maisha halisi ya mtoto na mazingira kabla ya kutoa hukumu.(SIR)
- x. Kusimamia huduma katika Mahabusi za Watoto ikiwemo kuwahifadhi na kuwatunza katika Mahabusi hizo ili kutoa ulinzi na usalama
- xi. Kushirikiana na jamii katika kutoa huduma muhimu za malezi na maadili mema kwa kuzingatia haki za watoto kwa lengo la kurekebisha tabia
- xii. Kusimamia huduma za marekebisho ya mtoto
- xiii. Kufanya uchunguzi wa kijamii katika mashauri ya watoto yaliyofikishwa mahakamani
- xiv. Kuwaunganisha watoto na vyuo vya ufundi stadi na kutoa rufaa katika maeneo mbalimbali ya huduma kulingana na mahitaji ya mtoto.

iii. Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu na Wazee

Huduma zitolewazo katika eneo hili ni pamoja na:

- i. Mafunzo ya stadi za kazi kwa watu wenye ulemavu
- ii. Huduma za unasihi na msaada wa kisaikolojia (Mental Health and Psychosocial Care and Support - **MHPSS**) kwa wazee na watu wenye ulemavu,
- iii. Matunzo kwa wazee na watu wenye ulemavu na wasiojiweza
- iv. Huduma ya utengemao kwa wazee na Watu wenye Ulemavu.
- v. Kuunda mabaraza ya wazee na kamati za watu wenye ulemavu
- vi. Kutoa nyenzo za kujimudu kwa makundi yote yenye uhitaji
- vii. kuratibu vyama, asasi, Kamati za watu wenye ulemavu na mabaraza ya Wazee
- viii. Kuwajengea uwezo wazee na watu wenye ulemavu ili waweze kuanzisha shughuli za kiuchumi
- ix. Kuhakikisha kunakuwa na mazingira rafiki ya kibiashara kwa watu wenye ulemavu
- x. Kutenga maeneo rafiki ya uchangamshi kwa ajili ya wazee na watu wenye Ulemavu.

- xi. Kuwezesha upatikanaji wa huduma za afya kwa Wazee na Watu wenye ulemavu wasiojiweza kwa kutenga madirisha ya Wazee katika vituo vya kutolea huduma na kutoa kipaumbele kwa makundi haya maeneo yote ya huduma za jamii.

HUDUMA ZA MFUKO WA AFYA YA JAMII CHF ILIYOBORESHWA (IMPROVED COMMUNITY HEALTH FUND – iCHF).

Huduma zitolewazo.

Uandikishaji Wanachama wa mfuko wa iCHF

Mahali pa kujiandikisha kuwa Mwanachama wa iCHF na gharama za kujiunga.

Matibabu yanayopatikana kupitia Bima ya Afya ya iCHF

Vituo/ Hospitali zinazotumia Bima ya Afya ya iCHF

Uhai wa Uanachama wa mfuko wa iCHF